



# Kumfuata Yesu huko INDONESIA



## Kuhusu Therahimi

**KUTANA NA TERAHIMI!**



**MIKA:** 11

**ANATOKEA:** Java Magharibi, Indonesia

**LUGHA:** Kiindonesia

**MALENGO NA NDOTO:**

- 1) Kuwa Afisa wa Polisi.
- 2) Kujifunza kutengeneza mipangilio ya maua.
- 3) Kusoma Kitabu chote cha Mormoni.

**FAMILIA:** Therahimi, Mama, Baba, dada mmoja na kaka wawili.

ILLUSTRATIONS BY STELIYANA DONEVA

## Jinsi Therahimi Anavyomfuata Yesu

“Ninapenda kuwasaidia wazazi wangu katika njia ndogo ndogo,” Therahimi anasema,” Anawasaidia wakati anaposafisha chumba chake na kutandika kitanda chake kila asubuhi. Pia anawasaidia kufagia na kupiga deki sakafu ya nyumba yao.

“Kuwahudumia wazazi wangu kunanifanya nihisi furaha sana,” anasema Therahimi. “Ninaonesha upendo wangu kwa Yesu Kristo kwa kuwasaidia wao.”



## Wewe Pia Unaweza Kumfuata Yesu!

Kuna njia nyingi za kumfuata Yesu. Je, ni kwa namna gani wewe unamfuata Yeye? Andika na utuelezee!



## Mambo ayapendayo Therahami

**HADITHI YA MAANDIKO:**  
Wakati Yesu alipozaliwa Bethlehemu



**MAHALI:**  
Ufukoni



**MATUNDA NA MBOGA MBOGA:**  
Ndizi, matikiti maji, karoti na brokoli

**RANGI:**  
Nyekundu na bluu



**SOMO SHULENI:**  
Hisabati